

## SOCIAL STUDIES STANDARD FOUR

### SEHEMU A

1. **Chagua herufi ya jibu sahihi na uandike kwenye nafasi uliyopewa**
  - i. Rais wa sasa wa Tanzania anaitwa nani?  
 (A) DR John Pombe Mgufuli (B) DR Samia S. Hassani (C) Dr Jakaya Mrisho Kikwete (D)  
 Mh Benjamini Mkapa [ ]
  - ii. Shughuli zipi kati ya zifuatazo hufanywa na watu wa mjini?  
 (A) Biashara na uchimbaji wa madini (B) Usafirishaji na biashara (C) Kilimo na ufugaji  
 (D) Kilimo na shughuli za viwanda [ ]
  - iii. Bwana na Bi Kyeju wanaishi na watoto ambao sio wa kuwazaa. Je hii ni aina gani ya famillia.  
 (A) Familia ya mke na mume (B) Familia ya yatima (C) Familia ya kuasiri  
 (D) Familia pana [ ]
  - iv. Wanafunzi watano A, B, C, D na E waliambiwa watofautishe kati ya muongo na karne. Yupi alikuwa sahihi kati ya hao.  
 (A) Karne ni miaka 10 wakati muongo ni miaka 100 (B) Muongo ni miaka 1000 wakati karne ni miaka 100 (c) Karne ni miaka 50 wakati muongo ni miaka 100 (D) Muongo ni miaka 10 wakati karnen ni miaka 100 [ ]
  - v. Jotoridi ni kiwango cha ubaridi au joto lililopo kwenye sehemu au kitu. Ipi kati ya ifuatayo kinachotumika kutambua kiwango cha jotoridi.  
 (A) Izothemo (B) Kipima joto (C) Zebaki na pombe (D) Nyuzi za sentigredi au nyuzi za farenihaiti [ ]
  - vi. Ali ni mtaalamu wa kuchora ramani mbalimbali, hivyo Ali ni?  
 (A) Mtabiri wa hali ya hewa (B) Mchoraji (C) Katografia (D) Mpaka rangi [ ]
  - vii. Kwanini ni muhimu kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria  
 (A)Kusahau yaliyopita (B) Kukumbuka yajayo (C) Kufundisha kizazi kipyambo yaliyopita  
 (D) Kuongeza idadi ya matukio [ ]
  - viii. Ipi kati ya zifuatazo si faida ya kuwa na mbuga za wanyama na misitu?  
 (A) Kupata nyama pori (B) Kulina asali (C) Kutoa ajira (D) Kuongeza ujangiri [ ]

**1. Oanisha kifungu cha maneno kutoa orodha A kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka kifungu B**

NO	FUNGU A	MAJIBU	FUNGU B
i.	Shughuli zinazofanywa sehemu za maziwa na bahari	[ ]	A. Tiketi za magari
ii.	Shughuli zinazofanyika sehemu zenye nyasi nyingi na malisho	[ ]	B. Ufugaji
iii.	Shughuli zinazofanya sehemu zenye mvua za kutosha	[ ]	C. Kilimo

iv.	Shughuli zinazofanywa sehemu zenyenye madini	[ ]	D. Seremala
v.	Shughuli zinzafanya maeneo yenye misitu	[ ]	E. Kuongoza mitambo
vi.	Sehemu zinazofanywa maeneo yenye mbuga za wanyama	[ ]	F. Uvuvi G. Utalii H. Ujangili
			I.

## SEHEMU B

### 2. Soma habari kwa makini kisha jibu maswali yafuatayo

John na fadhila ni wanafunzi wa shule ya msingi Methodius iliyyopo kijiji cha Kagongwa. Kijiji hicho hupata mvua za mara kwa mara. Kijiji cha Kagongwa kimezungukwa na ziwa Poma, mito na misitu minene. Wakati wa jioni Fadhila na John hupendelea kufanya mazoezi kwenye uwanja ambao upo karibu na nyumbani kwao.

Siku moja Fadhila na John walienda uwanajani wakiwa na nguo zao za michezo, ghafla Fadhila aligundua mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yalionesha dalili ya kunyesha kwa mvua. Kulikuwa na baridi na giza kwa sababu anga lilikuwa limefunikwa na wingu zito. Fadhila akainua kichwa na kuangalia juu. Anga lote lilikuwa limetandwa na wingu kwa upande mwingine wingu lilikua zito na jeusi. Radi zilisikika kutoka mashariki, kasi ya upepo ikaongezeka kuvuma kutoka upande ambao mvua ilikuwa inanyesha.

#### Maswali

- i. Kutokana na habari uliyosoma, Taja dalili moja ya mvua \_\_\_\_\_
- ii. Kwa nini kijiji cha kugongwa hupata mvua mara kwa mara \_\_\_\_\_
- iii. Fadhila alifanya nini kabla ya mvua kuanza kunyesha \_\_\_\_\_
- iv. Taja faida (2) za mvua katika mzingira yetu.
  - (a) \_\_\_\_\_
  - (b) \_\_\_\_\_
- v. Kipi kinafaa kuwa kichwa cha habri hii \_\_\_\_\_
- vi. Taja matumizi ya maji ya mvua \_\_\_\_\_

### 3. Changuzza kwa makini picha kisha jibu maswali yafuatayo



i. Shughuli zipi zimesababisha hali hii iliyoonesha kwenye picha.

ii. Hali ya wanyama kufa kwa ukosa maji na chakula kama ilivyooneshwa kwenye picha  
hujulikana kama \_\_\_\_\_

iii. Njia ipi utatumia kuokoa maisha ya viumbe hai waliopo kwenye eneo hilo\_\_\_\_\_

iv. Ni athari zipi zitawapata watu wanaoishi katika maeneo kama hnayo yaliyo kwenye  
picha\_\_\_\_\_